



Bwana wetu Yesu Kristo asifiwe, karibu ujifunze kwa kupitia ndoto.....

Mara nyingi ndoto tuotazo huwa zinakuja kwa shughuli nyingi..lakini ikitokea imekuja kwa uzito kidogo, basi yakupasa utafute maana halisi...

Kuota mti au kuuona mti kwenye ndoto kuna maana nyingi kulingana na ujumbe ambao Bwana anataka kuufikisha, maandiko yameeleza wazi nini maana ya mti...

Marko 8:24

[24]Akatazama juu, akasema, Naona watu kama miti, inakwenda.

Maana yake mti kibiblia unawakilisha mtu, na kama umeona umeanguka ni ishara ya kuanguka/anguko la Kimwili, uchumi, kiafya, au ni kifo moja kwa moja pamoja na Kutengwa na uso wa Mungu.....

Kama ulishawahi kuiota hiyo ndoto au umeiota basi jiangalie sana mara mbili...

Danieli 4:20-22

[20]Ule mti uliouona, uliokua, ukawa na nguvu, urefu wake ukafika mpaka mbinguni, na kuonekana kwake mpaka dunia yote;

[21]ambao majani yake yalikuwa mazuri, na matunda yake mengi, na ndani yake chakula cha kuwatosha wote; ambao chini yake wanyama wa kondeni walikaa, na ndege wa angani walikuwa na makao yao katika matawi yake;

[22]ni wewe, Ee mfalme, uliyekua, na kupata nguvu; maana ukuu wako umekua na kufika mpaka mbinguni, na mamlaka yako yamefika mpaka mwisho wa dunia.



Tubu leo dhambi zako kwa kumaanisha kuziacha kabisa ili anguko hilo lisikupate na kisha ukabatizwe ubatizo sahihi wa maji mengi na kwa Jina la Yesu na umgeukie Bwana.,,

Bwana wetu anakuja.....

Mada zinginezo;

KUOTA UNALISHWA VITU AU UNAKULA VITU.

KUOTA UMECHELEWA KWENYE HARUSI.

MAANA YA KUOTA UNAFANYA MAPENZI.

KUOTA UNAOKOTA HELA